*Jiwe la kiroho la kujenga No 45*

# Ulimwengu katika uchungu WA kuzaa.

Warumi 8:22-23, "Kwamaana twajua ya kwa viumbe vyote. Pia vinaugua pamoja, navyo vinauchungu pamoja pamoja hata sasa. Wala si hivyo tu, ila sisi wenyewe tulio na malimbuko ya Roho, sisi. Pia tunaugua katika nafsi zetu, tukitazamia kufanywa wana. Yaani ukombozi wa mwili wetu"

Tunamshukuru sana kwa neno la unabii kwa saa hii "Nasi tunalile la unabii lililoimara zaidi, ambalo, mkiliangalia kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya nyema, mpaka kutakapo pambazuka,na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu." (2petro 1:19) sasa, zaidi maneno ya ndugu Branham, Nabii wa Mungu kwa siku ambayo tunsihi.

Ulimwengu uko kwenye utungu wa kuzaa sasa. Cha zamani kinapaswa
Kufanya vile vile pia, hivyo kipya kinaweza kuzaliwa. Kama tu vile mbegu inapaswa kuozelea mbali ili kutoa uhai mpya (Yohana 12:24) na maumivu jinsi gani, uchungu wa kuzaa umeipiga dunia! Katika vita vya kwanza ya dunia, yeye alikuana maumivu makubwa kwa sababu walikua na gesi ya sumu, nakadhalika hivyo karibuni vingeweza kuaribu ulimwengu. Na katika vitu ya pili ya dunia yeye alipigwa tena, maumivu makali : kulikua na mlipuko mkubwa na pia bomu la atomiki. Yeye hawezi tena kuhimili umimivi juu ya maumiv. Pamoja na makombora haya na mambo/ vitu moja zaidi itamtoa yeye kutoka katika nafasi, kwakua yeye sasa ataokolewa. Na kutakua na dunia mpya (Isaya 65:17-25). Biblia ilisema itakuwapo.

Chini ya kila ujumbe wa kila nabii. Israel walipata uchungu wa kuzaa, kwasababu manabii hawa wangekuja baada ya wanatheolojia na mapadri ungekuwa na kanisa katika mfumo wa shirika. Na wakati manabii wao walipo kuja na HII ASEMA BWANA, walichochea makanisa yao na alikua na uchungu wa kuzaa. Hatimaye, alikua na maumivu ya kuzaa mpaka alizaa mwana wa Injili,ambaye alikua ni neno lenye likifanyika mwili (Yohana 1:1-3,14)

Hivyo kanisa kwa hakika liko katika uchungu wa kuzaa leo tena, kwa ajili ya kumzaa mwana, mwana wa Mungu kuja tena. Yote ya theolojia yetu, yote ya mifumo yetu, yote ya madhehebu yetu, imeoza kutoa ahili yetu. Hivyo tuko katika uchungu wa kuzaa na ujumbe kutoka kwa Mungu kila mara hutupa kanisa maumivu makubwa zaidi, lakini baada ya muda yeye anaenda kumzaa bibiharusi. Na hiyo itamleta Yesu kristo kwa bibi harusi wake. [1]

Angalia, sura ya 13 sasa, ya Isaya. Hebu na tuanze hapa kwenye aya ya 6.
“Pegeni kilele za hofu, maana siku ya Bwana ikaribu itakuja kama maangamizi yatokayo mwenyezi Mungu”

Angalia muhuri huu wa sita ukifunguliwa hapa sasa. Moja kwa moja huku nyuma, miaka miasaba na kumi na tatu (713) kabla kristo hajaja. Naye amekaa miaka 2000: hiyo ingekua Kama miaka 2700 iliyopita Isaya auliuona muhuri huu ukiningiinia pale. Vema.

“Kwasababu hiyo mikono yote italegea na moyo wa kila mtu utayeyuka” Yesu alisema nini? “na kwasababu ya kuongezeka kwa maasi, upande wa winge utapata (Mathayo 24:12). Na mioyoni ya watu itavunjika, kwa hofu, bahari ikivuma” (Luka 21:25-28) unaona, mioyo ya watu italegea.

“Nao watafadhaika, watashikwa na uchungu na maumini watakuwa na uchungu kama mwanamke aliye karibu na kuzaa, watakodoleana macho, nyuso sao zitakuwa za aibu”.

Angalia jambo hilo tena hapa, hoo, “nyuso zao zimeaibika” tutashikilia hilo. “Tazama siku ya Bwana inakuja, siku kali, ya hasira na ghadhabu kuu, ili Iifanye nchi kua ukiwa, naye atawaharibu watu wake mwenye dhambi, maana nyota za mbinguni na matangamano havitatoa nuru yake, jua litatiwa giza wakati wa kujaa kwake kwa mwezi utaacha nuru yake isiangaze. Nami Nitaadhibu ulimwengu kwasababu ya ubaya wao, na hatia, na uovu kwasababu ya hatia yao,name nitakomesha fahari yao wenye kiburi nami nitayaangusha chini majivuno yao waliowakali” ( Isaya 13:6-11)

Unaona hapo, hiyo ni sawa, Isaya aliona jambo lile lile ambalo Yesu alinena habari zake. Ambalo muhuri wa saba unafunua. Wakati anaisafisha nchi kwa ile dhiki, huona wakati anaisafisha nchi kwa ile dhiki, huo ni wakati wa ile dhiki, huu muhuri wa sita, naam, Yeye alikuwa ni nabii, naye alijulishwa neno la Mungu.Hiyo ni miaka 2700 iliyopita.

Kweli! Ninataka tu kusema jambo hili. Ulimwengu mzima Kaman tu vile Isaya hapa…….. Kama uchungu wa mwanamke aliyekaribu kuzaa, viumba vyote vinaugua. (Yohana 16:21-22). Kuugua kote huku na utungu wote ni kwanini, kwasababu gani, kama mwanamke aliyekaribu kuwa mama, dunia yenyewe….maumbile?

Angalia hilo, siyo hapa tu ulimwengu wote, na mambo yauchafuayo ulimwengu

, Maumbile…… Mungu aturehemu ulimwengu wote na utungu wake wa kuzaa, Ulimwenghu unaugua. Isaya alisema kuna nini? Anajaribu kuleta ulimwengu mpya kwa ule utawala wa miaka elfu ambapo dhambi zote zimetupwa nje, anajaribu kuzaa ulimwengu mpya kwaajili ya watu wapya ambao watatenda dhambi na kuuchafua. Hiyo ni sawa, unaugua. Hiyo ndiyo sababu tuko katika kuugua. Kristo kuleta bibi harusi. Kila kitu kinaugua na kutaabika. (Warumi 8:22-23) unaona, kuna kitu kinakaribia kutukia na pigo la sita linaachilia uende ndugu,tetemeko la ardhi linapasuka, na nyota zinatingishika volakano zitakuja, na dunia itajilipika kutoka katikati ya dunia…………..

Na nawaambia, Asubuhi moja wakati Yesu na Bibi Harusi wake wakati atakapokuja duniani, kutakuwa na Paradiso ya Mungu palr hiyo……….. (Ufunuo 1:11-16) oh,jamani. Hao mashujaa wakale wa vita wakitembea chini pale na rafiki zao na wapendwa wao, nyimbo za utukufu zitajaza anga, za muaminifu, ingia katika furaha ya Bwana ambayo imeandaliwa kwa ajili yako kama ile ingekuwa kule nyuma kala hawajaanzisha mpira kuzungua ndani ya dhambi" (Mathayo 25:21) Amina.

Ndiyo, muhuri wa sita unaenda kufanya kitu Fulani. Ndiyo Bwana, hakika ulimwengu wote unataabika na kuumia kwaajili ya utawala wa miaka elfu. Ni wakati kwa muhuri wa sita, kwa kufunguliwa, na wakati akifanya, oh jamani…..Mwisho chukuwa nafasi yake. Yeye anaenda sasa kuolewa na mfalme. Wakati hili likiendelea na mabali ya Israeli wanatia muhuri tayari kwa kwenda (Ufunuo 7:1-8) na halafu maumbile wacha yaendelee. Oh!, ni wakati wa aina gani. [2].

Tunaambiwa na nabii wa Mungu kwamba tunakuwa na dunia mpya, mbingu mpya na ulimwengu mpya. Kama unataka maandiko ya hayo. Ni ufunuo 21:1 Yohana alisema "ni kaona kama mbingu mpya na nchi mpya, kwa maana mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza imekwisha pita." Ilikuwa imeondoka. Sasa, kama tutakuwa na nchi mpya, nchi zamani na nchi mpya haiwezi kudumu katika wakati uleule. Au , ulimwengu mpya na wazamani haviwezi kudumu kwa wakati mmoja. Hakuwezi kuwepo na taratibu mbili za ulimwengu kwa wakati mmoja. Sasa, ili upate nchi mpya ya zamani unapaswa ite. Sasa, kama ile ya kale inapaswa kufa, basi inapata uchungu wa kuzaa kwajili ya ile mpya sasa.

Moja ya vitu vya kwanza amabayo daktari anafanya baada ya kumuangalia mgonjwa ni kupima muda wa uchungu wa kuzaa. Yeye anapima muda wa uchungu, jinsi inavyokaribiana pamoja na jinsi kila mmoja unavyopata uchungu zaidi. Mmoja ni mkali kuvumilia kuliko huwo mwingine. Unafuwata, mkali zaidi, unakuwa karibu zaidi na mwingine. Hivyo ndivyo hupima hali hiyo, kwa uchungu wa kuzaa.

Vyema, kama ulimwengu hauna budi kuondoka kusudi ulimwengu mpya upate kuzaliwa, hebu na tuchunguze baadhi ya uchungu wa kuzaa tulio nao duniani, ndipo tutaona tupo katika siku gani nayo imeenda umbali gani katika uchungu wake.

Vita vya kwanza vya dunia iliyooneyesha utungu mkubwa sana wa kuzaa. Ilionyesha moja ya utuungu wa maumivu ya kwanza kwenda katika kuzaa wa kuingia kwake katika utuungu wa uzazi kwa sababu ya wakati ule kwake, tulikuwa tumeleta mabomu. Na tulikuwa na mashine gani, tulikuwa na gesi ya sumu, dunia iliingia katika utungu wake wa kwanza wa kuzaa. Na tunaona ya kwamba sasa tulikuwa na vita kuu ya pili na utungu wake ulikuwa na maumivu makali wakati ule maumivu ya kuzaa kwa dunia ilikuwa karibu azae wakati ule kwa sababu kulikuwa na mabomu yaliyokuwa na uwezo wa kuharibu mji mzima ilikuwa ni maumivu makali kuliko yale yaliyokuwa katika vita vya kwanza kwani kulikuwa na uharibifu mkubwa duniani. Sasa dunia inajua kwamba wakati wake wa kuzaa umefika ndiyo maana dunia imechanganyikiwa na mazingira yaliyopo kwa sababu sasa hivi kuna mabomu ya hydrogen kuna mabomu yakuweza kushusha kutoka bara moja kwenda bara nyingine ambayo yanaweza yakaharibu dunia yote. Taifa moja linaogopa taifa linguine haijalishi hata ni kadogo kiasi gani wanaweza wakaziongoza zikaanguka kwenye lengo hasa wanakotaka wapigwe. Sayansi ya wanadamu imeingia katika laboratory ya Mungu mpaka wamefikia kiwango cha kuweza kujiangamiza wenyewe. Mungu kwa kawaida huachia hekima ya wanadamu ijiangamize wenyewe. Mungu huwa haaribu chochote mwanadamu anajiaribu kwa hekima yake mwenyewe kama alivyofanya pale mwanzoni kwa kuchukuwa hekima ya shetani badala ya Mungu. Sasa hivi najuwa kwamba nilazima iangamie haiwezi kustahimili tena .

Kwahiyo dunia inajua kwamba haiwezi kustahimili utungu mkubwa wa uzazi itabidi iende kuzaliwa upya tunaenda kuzaliwa upya kule kuzaliwa upya kuko karibu ninashukuru kwaajili ya hiyo nimechoshwa nah ii moja tulionayo. Kila mtu anajuwa kwamba hapa ni mahali pa kifo na huzuni na mambo yote mabaya ninafurahi kwamba inabidi itoweke ninafurahi kwamba wakati umekaribia kama

Yohana wa zaman alivyosema hata hivyo na uje Bwana Yesu (Ufunuo 22:16-17, na mstari wa 20).

Sasa ni lazima ioze kwasababu nimesema ili kuuleta uzazi mpya angali kile inachopitia kwamba lazima ioze. Ndugu zangu wapendwa dunia imeozeana siasa zake na taratibu zake zimeoza kwa kadri ziwezavyo kuwa hakuna kitu kilichobaki ndani yake katika utaratibu wa dunia siasa zake, dini zake, siasa zake, chochote kile kiwacho kitu chote hichi kimeozeana kabisa lazima kuwe na kitu kingine kitakachochukuwa mahali pake dunia haiwezi kusimama. Kama utachukuwa mtu kama George Washton au Abraham Lincolin katika nchi zote kama vile America haiwezi tena kurudi mahali pake, haiwezi kukombolewa. Kuna jambo moja tu la kuweza kuisaidia dunia ni kule kuja kwa Muumba wake Amina.

Inajuwa kwamba inabidi ihame iko kwenye utungu, iko kwenye maumivu. Hakuna hata mmoja anayejuwa cha kufanya kila mmoja anaangalia upande huu na mmoja anaangalia upande ule. Mmoja anamuogopa mwingine mmoja anajaribu kufanya kitu kitakacho mharibu mwingine na huyu mmoja anajaribu kumpinga huyu mwingine akimharibu mwingine mpaka sasa hivi vitu hivi viko mikononi mwa watu wenye dhambi ambao wanaweza wakaiaharibu dunia yote kwa dakika tano tu. Kwahiyo inajuwa haiwezi kustahimili tena watu wanajuwa haiwezi kusimama tena na dunia inajuwa kwamba inaelekea kwenye tukio hilo ambalo ni la uharibifu kwa maana Mungu amesema itakuwa hivyo . Mbingu zote na dunia zitaenda kuwaka moto zitaenda kufanywa upya ili dunia mpya iweze kuzaliwa Mungu amelitabiri hilo (2 Petro 3:8-10) imeoza katika taratibu zake zote , na itabidi ifanyike hivyo kwasababu imeozeana ndio maana imechanganyikiwa ikiwa na uso mwekundu na kuchanganyikiwa na kuwa na hofu na matetemeko ya ardhi kila mahali yakitokea katika pwani zote na mawimbi makubwa yakitetemesha juu na chini katika Pwani matetemeko ya ardhi na mambo mengineyo na watu wakijiuliza tuondoke mahali hapa unaona? Hawajuwi cha kufanya hakufana mahali palipo palipo salama ila mahali pamoja tu ni kuwa ndani ya Kristo mwana wa Mungu aliyehai. Vyote vilivyo nje ya huyo vitaangamia kwa hakika kabisa sababu Mungu amesema hivyo .

Sasa Yesu alituambia kwa uhakika kile kitakachotokea kwa uhakika wakati huu alituambia katika mathayo 24 kwamba kanisa la asili na kanisa la kiroho yatakuwa karibu sana (Wagalatia 4:21-31) – waigizaji mpaka wataweza kuwadanganya hata wateule kama inawezekana (Mathayo24:24) Jinsi ilivyokuwa hivyo siku za Nuhu walikuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa na umomonyoko wote huu wa maadili uliopo duniani ambao tunauona leo duniani (Luka 17 :26-30) Ile biblia

kitabu cha daktari kinasema kwamba hilo litatokea na linasema kwamba tunapoliona hilo tunajuwa kule kuzaliwa kuko karibu lazima iwe hivyo. Njoo Bwana. Sasa tunaangalia hilo siyo tu kwa taifa ni dunia yote. Sasa Izraeli kanisa hebu tuanze pale nyuma kwa dakika chache. Israeli walikuwa na utungu wa kuzaa kila mahali alipokuja nabii duniani. Walikuwa na utungu wa kuzaa kwa ujumbe wake alioutoa ulifanya nini? Nabii alikuwa na neno na alikuta mazingira wakiwa wamepanda uozo mwingi na taratibu nyingi katika watu mpaka nabii huyu alitingisha mpaka kwenye misingi yao walichukiwa na kila mtu kwahiyo Mungu anapotuma nabii, kanisa lenyewe linaingia katika utungu wa kuzaa kwasababu neno la bwana linakuja kwa nabii na yey pekee (Amosi 3:6-7) hilo ni neno lilonenwa kwa siku ile likadhihirishwa na nabii wa wakati huo siku zote imekuwa hivyo na ma Kanisa yalijenga taratibu zao nyingi kulizunguka hilo neno. Alikuja na kulitingisha sana alipokuja likawa na utungu wa kuzaa ilikuwa ni nini kurudi kwenye neno! rudi kwenye uhai! Taratibu hazina uhai. Ni neno la Mungu peke ambalo lina uhai (Yohana 6:63) taratibu zilizojengwa juu ya neno hazina uhai. Ni lile neno ndilo linalota uzima au uhai ule ujumbe uliwatingisha mabaki warudi kwenye neno kundi dogo litatoka na kuamini. Wakati wa nuhu ilikuwa ni watu nane tu (Mwanzo 10-16) Lakini iwavyo vyote Mungu alitingisha yale mabaki na aliangamiza waliobaki [3].

Sasa nataka uone hili kulikuwa na kusudi lenye sehemu tatu katika muhuri wa sita kulikuwa na kusudi lenye sehemu tatu la wale wapanda Farasi. Kila mala kumekuwa na kusudi lenye sehemu tatu katika haya mambo hilom linaturudisha nyuma kwenye 3 na 7. Mihuri 7 mapigo 7, nakadhalika. Sasa katika hizi 3 na hizi 7 ni namba za mahesabu ya Mungu katika kufunuwa neno lake. Sasa ukiangalia hata wale wapanda farasi kulikuwa na wapanda Farasi watatu 1 alikuwa mweupe mwingine alikuwa mwekundu na mwingine alikuwa mweusi . Sasa na Yule Farasi wa nne ni kitu gani ilikuwa ni mchanganyiko wa wale wa tatu pamoja unaona? Kusudi lenye sehemu 3 (ufunuo 6) sasa tunaona pia katika muhuri huu wa sita ukiwa umefunguliwa ilikuwa na makusudi 3 na haya makusudi ni haya: kusudi la kwanza ilikuwa ni kwamba mwanamali (mpumbavu) aliyelala inabidi apitie kwenye dhiki kuu ili kutakaswa (Mathayo 25:1-13) Ilibidi atakaswe dhambi zake za kutokuamini na kukataa ujumbe hili litafanyika wakati wa kipindi kile cha dhiki unaona wanaishia hapa kwenye ufunuo 7 , kati ya sura ya 6 na sura ya 7 tunamuona akiwa ametakaswa na tunamuona amepewa vazi jeupe
(ufunuo 7:13-17).

Sasa huyu hapa siyo bibi harusi lakini ni kanisa ni watu wasafi lakini hawakupata nafasi ya kupokea huo ujumbe au kwa njia moja ama nyingine walipotoshwa na

hao ma nabii wa uongo na hawakupata nafasi na bado ni watu waaminifu moyoni na Mungu anajuwa mioyo yao, na wako hapa wakiwa wametakaswa wakati ule angalia wakati mwingine wa kutakaswa hapa kwaajili ya wale wa Israeli waliokusanyika hilo ni kusudi la pili Mungu anawatakasa wa Israeli katika wakati wa dhiki kuu kati ya mamilioni waliokusanyika pale utakuwa na mia moja arobaini na nne elfu waliochaguliwa na wao wataenda kutakaswa (Ufunuo 7 :1-8; Danieli 12:1-3) Mungu anawatakasa Israeli.

Angalia hii dunia yote inabidi tena itakaswe (Ufunuo 6:12-17) utakuwa na mambo kama vile mwezi, nyota na vitu vyote vya asili kutakaswa (Mathayo 24:29-31) Unaona ni kitu gani dunia inaenda kujifanya upya yenyewe kwakutakaswa inajiweka tayari kwaajili ya utawala wa miaka elfu unakuja na kila kitu kilichokichafu inabidi kitakaswe katika muhuri wa sita. Sasa unaona kufunguliwa kwa huu muhuri wa saba nako kuna kusudi lenye siri tatu hii moja nitaizungumzia nayo imezungumza naiyo ni siri ya zile ngurumo saba (Ufunuo 10:1-7) Zile ngurumo 7 kule mbinguni zitafunuwa siri hiyo. Itakuwa ni wakati hasa wa kuja kwa Kristo, kwa sababu Kristo alisema hakuna anayejuwa ni wakati gani atarudi (Mathayo 24:36) [4]

Na sasa tunajuwa tunafahamu dunia imepita katika utungu wa uzazi mkubwa na kanisa linapita katika wakati wa utungu wa kuzaa. Kila mmoja wa hawa manabii walipokuja duniani ilikuwa ni utungu wa kuzaa kwa kanisa. Dunia imepitia vita kuu ya kwanza , vita kuu ya pili ya dunia na sasa hivi iko tayari kwaajili ya vita kuu ya tatu ya dunia. Inapitia kwenye utungu tena wa kuzaa. Lakini kuna jambo moja ambalo linaweza likaleta amani na hilo ni Kristo. [5].

Sasa vita kuu ya kwanza ya dunia vita kuu ya pili ya dunia kwa sasa hivi tuko tayari kwaajili ya vita kuu ya tatu ya dunia hiyo inachemka kila mahali hiyo ni nini? Waisraeli wako katika nchi ya kwao wakimsubiri Mesia wao . Kanisa la watu wa Mataifa, Lutha, Wesri, na sasa ni wakati wa Pentekosti ambao wamekuwa vuguvugu na wametapikwa nje hiyo ni sawa wakati wa Pentekosti
(Ufunuo 3:15-18). Lakini pale kabla ya kuangamizwa kwa dunia Yesu alisema kama ilivyokuwa wakati wa Sodoma ndivyo itakavyokuwa wakati wa kuja kwa mwana wa Adamu (Luka 17:26-30) kwamba kanisa la watu wa mataifa litapokea nguvu zilezile, litapokea malaika Yule Yule, shahidi yuleyule ……. Hakika unaweza ukaona hilo liko wazi kadri linavyoweza kuwa na hata mtoto anaweza akaliona hilo. [6]

Kabla ya tone moja la maji kudondoka, Nuhu alikuwa ameshaingia kwenye . Kabla ya moto kuchoma Sodoma Loti alikuwa ameshaondoka. Baba, tunaamini, kabla ya

nguvu za Atomic hazija iangamiza dunia vipande vipande, Kanisa litakuwa limeondoka (1Wafesaloniki 1:9-10; Warumi 5:8-9) tunafurahi sana bwana.

Tunaweza tukaangalia juu mbinguni na kumuona mwana wa Adamu akiinuka kutoka kwenye kiti chake cha enzi akianza kuelekea duniani kwaajili ya unyakuo wa kanisa lake, Kama Rebecca alivyopanda juu ya Ngamia na akashuka kwenye Ngamia alipokaribia nyumba ya Abraham kule shambani alikutana na Bwana Harusi (Mwanzo 24:61-67) Ohh Mungu , na kanisa litakutana na Bwana Harusi pale hewani (1Wafesaloniki 4:13-17) Ohh tusaidie Bwana tupe utamu wa Roho Mtakatifu ondoa uchungu wote na tofauti zozote ndani yetu tuunganishwe kabisa na Roho Mtakatifu. [7].

Siku zote nimesema kwamba katika siku za Nuhu alikuwa kwenye safina kabla ya tone moja la mvua kuanguka Loti alitoka sodoma kabla ya Moto kuwaka (Luka 17:26-30) Na Kanisa litakuwa utukufuni kabla ya Bomu la atomic kuanguka hiyo ni kweli kabla Atomic hazijadondoka . [8]

Sasa huu ni wakati wa ujumbe wa malaika watatu duniani. Na unajuwa kile ambacho ni ujumbe wa malaika watatu; Unaendelea sasa katika siku yetu. Huu ni wakati wa kuruka kwa ujumbe wa malaika watatu, kama wewe ni msomaji wa Biblia (Ufunuo 8:13) kulikuwa na ole 3 zikifwata hilo (ufunuo 9:12) Wa kwanza ilitokea wakati wa vita kuu ya kwanza. Ya pili ilitokea katika vita kuu ya pili unajuwa kile ambacho tunakiendea sasa vyema tuko mwisho wa njia au mwisho wa barabara tulipo tunalazimika kwamba tupo wakati wa mwisho. Kwa muda gani sijui ; Hakuna anayejuwa. [9].


**<u>Nukuu za Kingereza</u>**

1. Leo haya maandiko yametimia (65-0219) aya 27-30
2. Ule muhuri wa sita (63-0323), aya (326-333,352-359).
3. Utungu wa kuzaa (65-0124), aya (86-106)
4. Ule muhuri wa saba (63-0324E) aya (380-391)
5. Unasema huyu ni nani? (64-1227) aya 59
6. Ile alama ya mnyama na muhuri wa Mungu (61-0217) aya E-53
7. Wakati wa kanisa wa Tiatira (60-1208) aya 7-9
8. Ufunuo sura ya 4 sehemu ya kwanza (60-1231) aya 170
9. Chapa ya Mnyama (54-0513) aya 30-32

Jiwe la kiroho la kujengea No.45  mpya 2010) kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa, Imekusanywa na Gerd Rodewald
Friedsfr.69,D-75328 Schomberg, Germany
www.biblebelievers, Fax(+49)72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*

*Box 553 Korogwe -  Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*